

**Cour  
Pénale  
Internationale**



**International  
Criminal  
Court**

Namba : ICC-01/04-02/06

Tarehe : 22/08/2006

Asilia : kifaransa

**CHUMBA CHA UTANGULIZI I**

Kinaundwa ifwatavyo :

Bwana mwamuzi Claude Jorda, Mwamumzi prezidenti  
Bibi mwamuzi Akua Kuenyehia  
Bibi mwamuzi Sylvia Steiner

Msajili : Bwana Bruno Cathala

**HALI NCHINI JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA KONGO  
KESI  
MWENDESHA MASHTAKA dhidi ya BOSCO NTAGANDA**

Yenyi mhuri wa siri

**HATI YA KUAMURU KUKAMATA**

Ofisi ya Mwendesha mashtaka :

Bwana Luis Moreno-Ocampo, Mwendesha mashtaka

Bibi Fatou Bensouda, Mwendesha mashtaka makamu

Bwana Ekkehard Withopf, Mwakilishi wa kwanza wa Mwendesha mashtaka

**Chumba cha utangulizi I cha Mahakama ya Kimataifa ya Jinai**

(« Mahakama »),

**KIKIONA** ombi la Upande wa mashtaka linalo malengo ya kutowa hati ya kuamuru kukamata Bosco Ntaganda, liliyo letwa tarehe 13/01/2006, na pia alama za ushuhuda na habari zingine zilizo tolewa na Upande wa mashtaka,

**KIKIONA** vifungu 19-1 na 58-1 vya Mkataba wa Roma,

**KWAKUWA** kulingana na uaminifu wa alama za ushuhuda na habari zilizo tolewa na Upande wa mashtaka, kesi inayohusu Bosco Ntaganda ni yenyi kuwa chini ya mamlaka ya Mahakama,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini ya kwamba vita vya kudumu vilitendeka pa Ituri toka mwezi wa saba 2002 hadi mwisho wa mwaka 2003 na kuendelea,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini ya kwamba toka mwezi wa saba 2002 hadi mwezi wa kumi na mbili 2003, wanamemba wa « Forces patriotiques pour la libération du Congo » (FPLC) walitenda mara kadhaa vitendo vya kuwakubali katika jeshi la waFPLC watoto wenyi umri chini ya mwaka kumi na tano ambao walipewa mafunzo katika kambi za mazoezi za waFPLC za Bule, Centrale, Mandro, Rwampara, Irumu, Bogoro na Sota,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini ya kwamba toka mwezi wa saba 2002 hadi mwezi wa kumi na mbili 2003, wanamemba wa FPLC walitenda mara kadhaa vitendo vya kuwatia kwa nguvu katika jeshi la waFPLC watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano ambao walipewa mafunzo katika kambi za mazoezi za waFPLC za Bule, Centrale, Mandro, Rwampara, Irumu, Bogoro na Sota,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini ya kwamba kunako muda huu umetajwa, wanamemba wa FPLC walishirikisha moja kwa moja na mara kadhaa, watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano kwa mapambano yaliyotukia pa Libi na Mbau mwezi wa kumi 2002, pa Largu mwanzo wa mwaka 2003, pa Lipri na Bogoro mwezi ya pili na ya tatu 2003, pa Bunia mwezi wa tano 2003 na pa Djugu na Mongwalu mwezi wa sita 2003,

**KWAKUWA** kuna pia hoja elekevu za kuamini ya kwamba siasa/ tabia inayo zahniwa kuwa ya Union des patriotes congolais (UPC)/ ya waFPLC, iliyokuwa ya kuwakubali kwenyi jeshi ao kuwatia kwa nguvu katika jeshi la waFPLC watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano na kuwashirikisha moja kwa moja kwa mapambano, ilitumiwa katika hali ya vita hapo Ituri na kwa ushiriki na hali hiyo,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini ya kwamba toka mwezi wa saba 2002 hadi tarehe 8/12/2003, Bosco Ntaganda akiwa makamu wa kiongozi mkuu wa majeshi (« chef d'état-major général adjoint ») ahusikaye na operesheni za kijeshi hiyo ikiwa ngazi ya tatu katika tabaka ya waFPLC aliwatii tu Thomas Lubanga Dyilo, aliye kamanda mkuu wa makamanda (« commandant en chef ») waFPLC na Floribert Kisembo huyu akiwa kiongozi mkuu wa majeshi (« chef d'état-major ») ya waFPLC. Alikuwa mkuu wa karibu wa makamanda wa sekta wa waFPLC na alikuwa na mamlaka ya kisheria na ya matendo juu ya makamanda wa kambi za mazoezi za waFPLC na makamanda wa waFPLC wafanyao kazi kwenyi maeneo mbalimbali,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini i) ya kwamba Bosco Ntaganda alitumia mamlaka yake juu ya waFPLC ili kuiweka katika vitendo siasa/mpango iliyoundwa na ngazi za juu za UPC/ za waFPLC, ambayo ilikuwa ya kuwakubali katika jeshi na kuwaweka kwa nguvu watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano katika jeshi ya waFPLC na kuwashirikisha moja kwa moja kwa mapambano, na ii) ya kwamba alijuwa majukumu yake kwenyi waFPLC katika kuiweka katika vitendo siasa hiyo,

**KWAKUWA** kuna hoja elekevu za kuamini ya kwamba Bosco Ntaganda alienda ziarani mara nyingi kwenyi kambi za mazoezi za waFPLC ambamo watoto wa umri chini ya myaka kumi na tano walipewa mafunzo ili wawe wanajeshi wa waFPLC na alishiriki moja kwa moja katika mashambulizi ambamo wanajeshi wa FPLC wenyi umri chini ya myaka kumi na tano walishiriki pia moja kwa moja,

**KWAKUWA** kutokana na sababu zinazotamkwa hapa juu, kuna hoja elekevu za kuamini kama Bosco Ntaganda ana dhima ya jinai zifwatazo kulingana na kifungu 25-3-a cha Mkataba :

- i) uhalifu wa vita kutokana na kuwakubali kwenyi jeshi watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano, unao adhibiwa na kifungu 8-2-b-xxvi ao kifungu cha 8-2-e-vii cha Mkataba ;
- ii) uhalifu wa vita kutokana na kuwatia jeshini kwa nguvu watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano, unao adhibiwa na kifungu cha 8-2-b-xxvi ao kifungu 8-2-e-vii cha Mkataba ; pia

iii) uhalifu wa vita kutokana na kuwashirikisha moja kwa moja watoto wenyi umri chini ya myaka kumi na tano katika mapambano, unao adhibiwa na kifungu 8-2-b-xxvi ao kifungu 8-2-e-vii cha Mkataba, KWAKUWA kulingana na kifungu 58-1-b cha Mkataba, kukamatwa kwa Bosco Ntaganda kunahitajika kwa muda huu ili kuwa hakika yakwamba atafika mbele ya Mahakama na kwamba hata zuia uchunguzi ao kuhatarisha utaratibu wake,

## **KWA SABABU HIZO,**

## **KINATOA**

Hati ya kuamuru kukamata BOSCO NTAGANDA, ambaye picha zinasindikiza andiko hili, ambaye anadhaniwa kuwa raia wa Rwanda na mwenyi umri karibu ya myaka makumi matatu na tano, anayedhaniwa kama alikuwa mbele ya tarehe 8/12/2003 makamu wa zamani wa kiongozi mkuu wa majeshi ahusikaye na operesheni za kijeshi za waFPLC, anayedhaniwa kama alitajwa kiongozi mkuu wa majeshi ya waFPLC tarehe 8/12/2003, anayedhaniwa kuwa siku hizi moja wa makamanda wa Mouvement révolutionnaire du Congo (MRC), jeshi la wanamgambo linalo endesha kazi zake katika wilaya ya Ituri na kandokando tangu mwanzo wa mwaka 2005, na ajulikanye pia kwa majina ya Bosco Tanganda, Bosco Ntaganda, Bosco Ntangana, Bosco Ntagenda, Bosco Baganda, Bosco Taganda na pia « le Terminator ».

Imeandikwa kwa kingereza na kifaransa, ni maandiko ya kifaransa ndiyo yanayo uaminifu.

*/ameweka saini/*

---

**Bwana mwamuzi  
Claude Jorda  
Mwamuzi prezidenti**

*/ameweka saini/*

---

**Bibi mwamuzi  
Akua Kuenyehia**

*/ameweka saini/*

---

**Bibi mwamuzi  
Sylvia Steiner**

Imefanyika siku ya pili tarehe 22/08/2006  
pa The Hague (Uholazi)